Mitandao @JAMVILAHABARI Jamvi la habari jamvihabari +255676807684 Email: jamvinews@gmail.com

GAZETI LAKO

# JAMVI LA HABARI

ISSN Na 2683 - 6548: Toleo Na. 2522 JUMATATU FEBRUARI 10, 2024 Bei Tsh. 1000 Kenya Ksh. 60 www.jamvilahabari.co.tz

# AHSANTE DK. SAMIA



>> **Wakuu** wa EAC, SADC wapata muafaka vurugu za DRC nchini Tanzania

>> **Asisitiza** kuwa DRC nchini mwanachama ni lazima kuhakikisha usalama wake

>> **Asema** hali ya mauaji na mateso inayoshuhudiwa katika nchi hiyo haikubaliki

## Dk.Biteko awaasa Waislamu kuhifadhi Qur'aan Tukufu .Uk.3



## DAWASA yamaliza shida ya Maji Tabata, Kinyerezi

NA JUMA KASESA

ZIMESALIA siku 10 tu kabla ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam(DAWASA) kumaliza tatizo la maji kwa wakazi wa Tabata,Segerea na Kinyerezi.

Wakazi wa maeneo wamekuwa kwenye kadhia ya ukosefu wa maji kwa muda mrefu lakini sasa ni rasmi tatizo linakwenda kumalizika baada ya DAWASA kukamilisha mradi wa upelekaji maji kwa maeneo hayo kwa asilimia 99.

Kaimu Mkurugenzi wa DAWASA,Mkama Bwire amewaeleza wananchi wa maeneo hayo kwamba kuanzia Februari 20 mwaka huu watafungulia rasmi maji ili

>> Inaendelea Uk. 3

## Wassira: Wakutatua kero za watanzania ni CCM

Uk.3



# AHSANTE DK SAMIA

NA MWANDISHI WETU

HATIMAYE Tanzania meendelea kuwa nchi inayoheshimika katika ukanda wa SADC, baada ya wiki hii kufanyika mkutano wa pamoja wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), kujadili na hatimaye kuchukua hatua kufutia mapigano yaliyoshika kasi katika eneo la Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Wakuu hao kwa kauli moja waliridhia mkutano huo kufanyika nchini Tanzania, chini ya Uenyeji wa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan, hatimaye umekalimika na kuondoka na maazimio 13 ikiwamo kusitishwa kwa mapigano mara moja katika eneo la Goma, Mashariki mwa nchi ya DRC.

Mkutano huo unakuja siku chache baada ya Tanzania kupokea ugeni mzito uliohusisha takriban Wakuu wa nchi takriban 23 pamoja na Mawaziri 60 na wadau wengine wa Maendeleo kwa ajili ya kujadili matumizi ya Nishati Bora Afrika.

Kwa pamoja heshima hizi zinatokana na juhudi za Rais wa Awamu ya Sita Dkt Samia Suluhu Hassan kuifungua nchini kimataifa na kuwa na ushirikiano mwema na nchi mbalimbali duniani.

Katika mkutano huo uliofanyika juzi Jumamosi Februari 8 na kuongozwa na kwa pamoja na Mwenyekiti wa EAC na Rais wa Kenya, Wiliam Ruto na Mwenyekiti wa SADC na Rais wa Zimbabwe, Dk. Emmerson Mnangagwa, uliendelea kuimwagia sifa Tanzania kwa utulivu na amani huku juhudi za viongozi wake wakiweka kipaumbele kuimarisha uchumi. Mkutano huo, uliohudhuriwa na Marais kutoka jumuiya hizo, ambapo masuala mengine waliyokubaliana ni pamoja na kurejesha huduma muhimu ikiwemo kufungua njia za usambazaji wa chakula na bidhaa nyingine, ili kuhakikisha misaada ya kibinadamu inawafikia walengwa bila kukwama.



Masuala mengine yaliyojadiliwa kwa kina ni utatuzi wa mzozo wa DRC pia kurejeshwa kwa amani kupitia mchakato wa Luanda na Nairobi, huku mkutano huo wa pamoja ukizingatia ripoti ya mkutano wa Mawaziri wa EAC na SADC, kuhusu hali ya usalama Mashariki mwa DRC na kusisitiza ushirikiano ya kisiasa na kidiplomasia ndiyo suluhisho endelevu zaidi la kutatua mzozo eneo hilo.

Mkutano huo wa pamoja umeagiza Wakuu wa Majeshi ya Ulinzi ya katika nchi za EAC na SADC, kukutana ndani ya siku tano na kutoa maelekezo ya kusitisha mapigano mara moja na bila masharti na kuondoa uhasama.

Aidha umesisitiza kutolewa kipaumbele kwa utoaji wa usaidizi kwa mahitaji ya kibinadamu ikiwemo kuwarejesha nyumbani marehemu na kuwahamisha waliojeruhiwa ili wakapate tiba sehemu salama.

Mjadala huo pia ulisisitiza kuendelezwa kwa mpango wa kuweka usalama kwa eneo la Goma na maeneo ya jirani, kama Sake Bukavu, Kibumba, Rumangabo, Kalengera Rutshuru, Bunagana, na Kiwanja Rwindi, Kanyabayonga, Lubero, pamoja na Ziwa Kivu kati ya Goma na Bukavu.

Kadhalika makubaliano yaliyofikiwa ni kufunguliwa tena mara moja kwa uwanja wa Ndege wa Goma na kushauri kuhusu afua zingine zinazohusiana na uwezeshaji.

Mkutano huo ulikumbusha tena jukumu muhimu la mchakato wa Luanda na Nairobi na kuagiza kwamba, mambo hayo mawili yaunganishwe na kuwa Mchakato wa pamoja

Pia uliazimia zaidi kuimarisha michakato hiyo miwili haraka, ili kuongeza utimilifu na kuwapa mamlaka wenyeviti wenza, kwa kushauriana na Umoja wa Afrika (AU).

Pamoja na Marais wa Kenya na Zimbabwe.

Mkutano huo umehudhiriwa na mwenyeji Tanzania, Rais Samia Suluhu Hassan, Rais FÈlix Tshisekedi wa DRC, Cyril Ramaphosa, Rais wa Afrika Kusini.

Wengine ni Paul Kagame, Rais wa Rwanda, Hassan Sheikh Mohamoud, Rais wa Somalia, Rais wa Uganda Yoweri Museveni, Rais wa Zambia Hakainde Hichilema, pamoja na vingozi wengine waliohudhuria ambao ni wawakilishi Marais kutoka Burundi, Malawi, Angola, Sudan Kusini, Madagascar pamoja na Mwenyekiti wa Tume ya AU, Faki Mahamat na Katibu Mkuu SADC, Elias Magosi na Katibu Mkuu EAC, Veronica Nduva.

# TRUMP ATIMUA RAIA 400 WA INDIA

NA MWANDISHI WETU

MAAFISA wa India wameripoti kuwa raia 104 wa nchi hiyo wamefukuzwa kutoka Marekani kwa kutumia ndege ya kijeshi ambapo hatua hiyo inakuja wakati masuala ya uhamiaji kati ya nchi hizo mbili yameendelea kuibua mijadala, huku wengi wa waliofukuzwa wakidaiwa kuingia nchini humo bila vibali halali.

Aidha ripoti zinaeleza kuwa baadhi ya waliorejeshwa walifungwa pingu wakati wa safari yao, hali iliyozua malalamiko kutoka kwa familia na viongozi wa kisiasa nchini India. Wabunge wa upinzani wametaka serikali kutoa maelezo kuhusu madai ya unyanyasaji dhidi ya raia hao wakati wa kurejeshwa kwao

Waziri wa Mambo ya Nje wa India, Subrahmanyam Jaishankar, amesema kuwa serikali inaendelea kushirikiana na Marekani ili kuhakikisha kuwa raia wa India wanaorejeshwa wanaheshimiwa haki zao. Ameeleza kuwa matumizi ya pingu kwa wahamiaji wanaorejeshwa yamekuwa sehemu ya utaratibu wa Marekani tangu mwaka 2012

Tukio hili limeongeza msukumo wa majadiliano kuhusu uhamiaji kati ya India na Marekani, hasa wakati viongozi wa mataifa hayo mawili wanapojiandaa kujadili masuala ya usalama na sera za uhamiaji katika mazungumzo yanayotarajiwa hivi karibuni

# Wassira: Atakayetatua changamoto za wananchi ni CCM

NA MWA NDISHI WETU

MAKAMU Mwenyekiti wa CCM Mzee Steven Wassira; amewaondoa hofu Wanachama wa chama hicho na wananchi kwa ujumla kuwa changamoto wanakutana nazo zinafahamika na Serikali inayoongozwa na CCM na kwamba hao pia ndiyo wenye jukumu la kuzitafutia ufumbuzi.

Mzee Wassira aliyasema hayo hivi karibuni katika mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM wilaya Rplya mkoa Mara ambapo aselima mfano wa changamoto za wiyala hiyo ni ujenzi wa barabara kwa kiwango cha Lami, changamoto ambayo tayari ipo katika mipango ya kutatuliwa.

Alisema kuwa CCM kazi yake pamoja na mambo mengine ni kusikiliza kero za wananchi na kuzifanyia kazi kwa vile kufanya hivyo ndiko kutakakoendelea kudumisha mahusiano mema ya wananchi na chama chao tawala.

Amewata wana CCM na wapenzi wa chama hicho kuendelea kuwa na mshikamano ili kuenzi juhudi za Rais wa Awamu ya Sita Dkt Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa mstari wa mbele kupigania maslahi ya wananchi.



# DAWASA yaja na mwarobaini tiba ya maji Tabata, Segerea

NA JUMA KASESA

ZIMESALIA siku 10 tu kabla ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam(DAWASA) kumaliza tatizo la maji kwa wakazi wa Tabata,Segerea na Kinyerezi.

Wakazi wa maeneo wamekuwa kwenye kadhia ya ukosefu wa maji kwa muda mrefu lakini sasa ni rasmi tatizo linakwenda kumalizika baada ya DAWASA kukamilisha mradi wa upelekaji maji kwa maeneo hayo kwa asilimia 99.

Kaimu Mkurugenzi wa DAWASA,Mkama Bwire amewaeleza wananchi wa maeneo hayo kwamba kuanzia Februari 20 mwaka huu watafungulia rasmi maji ili kuwaondolea kero hiyo ya muda mrefu.

Bwire alisema,serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Dk.Samia Suluhu Hassan imedhamiria kuwaondolea kero ya maji Wananchi wake kwa kutoa fedha za ukamilishaji miradi mbalimbali ikiwemo huo wa ambao unakwenda kuwa mwarobaini wa tatizo la maji kwa wakazi wa maeneo hayo.

# Dk.Biteko awaasa waislamu kuhifadhi Qur'aan tukufu

NA MWANDISHI WETU

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati,Dk.Doto Biteko amewaasa waislamu nchini kuendelea kumcha Mungu na kutenga muda wa kujifunza na kuisoma Qur'aan Tukufu ambayo itawafunza mambo mema yaliyoelekezwa na Mwenyezi Mungu.

Dk.Biteko aliyasema hayo jana jijini Dar es salaam wakati akizindua Mashindano Makubwa zaidi ya Qur'aan Tukufu Ulimwenguni 2025.

" Nawaomba msivunjike moyo akitokea mwenye tafsiri tofauti nyie msivunjike moyo wala kukatishwa tamaa bali mfanye mashindano haya yawe kinara na kuutangaza uislamu katika ulimwengu," amesema Dkt. Biteko.

Pia amewahimiza kumuomba Mungu ili Qur'aan iwanyanyue na isiwabwage katika shughuli mbalimbali wanazofanya kama kaulimbiu ya mwaka huu inavyosema " Qur'aan Ikunyanyue, Isikubwage".

Alisema,Qur'aan inatoa funzo kwa watu na kuwa waasisi wake waliyaanzisha kwa ngazi ya madrasa lakini baadaye kutokana na umuhimu wake yakavutia wengi zaidi na kuwa mashindano ngazi ya mtaa, kata, wilaya, mkoa hadi kuwa ya Afrika Mashariki, Bara la Afrika na kisha kufikia ngazi ya kuwa mashindano ya Ulimwengu.

" Mashindano haya mbali na kuwa yanachochea usomaji wa Qur'aan Tukufu na hivyo kujenga uelewa wa hofu ya Mwenyezi Mungu lakini pia yanaitangaza Tanzania katika taswira chanya," amebainisha Dk.Biteko.

Alisema,kuwa Nabii Musa aliwalingania watu wake kwa kutumia muongozo kutoka katika Taurati, Nabii Daudi yeye akatumia Zaburi, Nabii Issa (Yesu) akatumia Injili na Mtume Muhamad swalla llahu alayhi wasallam akatumia Qur'aan tukufu kuwalingania watu wa umma wake.

"Kimsingi vitabu hivi vya muongozo vinamfundisha binadamu tabia njema na kumsihi kuzishikilia na kumuonesha tabia zisizofaa na kumuasa kukaa mbali nazo."

Dkt. Biteko amerejea aya katika Qur'aan tukufu sura ya 35, Surat Faatir, aya ya 28 "… kwa hakika wanaomcha Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja wake ni wanazuoni".

Amefafanua " Aya hii ina maanisha kuwa wale waliopata ujuzi na mafundisho ya Mwenyezi Mungu ambayo yanapatikana katika Qur'aan tukufu na kuyazingatia yale waliyojifunza ndio wanaofika daraja la uchamungu."

Vilevile, Dkt. Biteko ameipongeza Taasisi ya Al-Hikma kwa jitihada zake za kukuza Mashindano ya kuhifadhi Qur'aan Tukufu ulimwenguni.

Mkurugenzi Mkuu wa Al- Hikma na Mwenyekiti wa Mashindano ya Qur'aan Tukufu Ulimwenguni, Sheikh Nurdin Kishk amesema kuwa mashindano hayo yameendelea kukua kila mwaka kutokana na mapenzi ya kuhifadhi Qur'aan.

Aidha, ameishukuru Serikali kwa ushirikiano wake na kwa kuridhia mashindano hayo kufanyika katika Uwanja wa Taifa Machi 16, 2025 ambapo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi anatarajiwa kuwa mgeni rasmi.

" Mashindano haya yanayofanywa na Al- Hikma Foundation yameweka alama ambayo haitafutika na mataifa mbalimbali yameanza kuyaiga. Pia, Mashindano Makubwa Zaidi ya Qur'aan Tukufu Afrika sasa yatajulikana kama Mashindano Makubwa Zaidi ya Qur'aan Tukufu kwa Mabara yote ya Ulimwengu ," amesema Sheikh Kishk

Akizungumza kwa niaba ya Mufti Mkuu wa Tanzania, Sheikh Ali Ngerukwa alisema kuwa Mufti Mkuu yupo tayari kushirikiana na taasisi mbalimbali ikiwemo ya Ali- Hikma katika kutekeleza shughuli zao.



# DKT SAMIA AWAHAKIKISHIA USHIRIKIANO EAC

NA MWANDISHI WETU

RAIS Samia Suluhu Hassan amewahakikishia Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kuwa Tanzania itaendelea kutoa ushirikiano katika kushughulikia mgogoro unaoendelea Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (DRC).

Aidha, Rais Samia ametoa rai kwa Jumuiya hizo mbili kuchukua hatua kuhakikisha kuwa DRC, ambayo ni mwanachama wa EAC na SADC, inakuwa salama na mgogoro unaoendelea nchini humo unamalizika.

Kwa mujibu wa taarifa ya Ikulu Rais Dk Samia ameyasema hayo leo wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa pamoja wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa EAC na SADC uliofanyika katika Ikulu ya Dar es Salaam ili kujadili hali ya usalama Mashariki mwa DRC.



Rais Samia alieleza kuwa hali inayoshuhudiwa Mashariki mwa DRC haikubaliki na ipo haja ya kuchukua hatua za haraka kumaliza mgogoro huo unaoleta mateso kwa wananchi.

Alisema ana imani kuwa Mkutano huo utatoka na maazimio ambayo yatawezesha wananchi wa Mashariki mwa DRC kuishi amani.

Kwa upande wake Rais wa Jamhuri ya Kenya, ambaye pia ni Mwenyekiti wa EAC, Dk William Samoei Ruto amesema mgogoro unaoendelea Mashariki mwa DRC hautamalizwa kwa kutumia silaha bali kwa njia za kidiplomasia kupitia mazungumzo, kusikilizana na kushauriana.

Aidha, amewataka wadau wote kushirikiana na EAC na SADC ili kumaliza mgogoro huo ambao unaendelea kugharimu maisha ya wananchi wasio na hatia.

Kwa upande wake Rais wa Jamhuri ya Zimbabwe na Mwenyekiti wa SADC, Dk Emmerson Dambudzo Mnangagwa amesema hali inayoendelea Mashariki mwa DRC inaathiri bara zima la Afrika, hivyo nchi za Afrika zinapaswa kushikamana kama zilivyoshikamana wakati wa kupigania uhuru wa bara la Afrika.

## Haya ndio maazimio ya Wakuu wa Nchi wa EAC na SADC kuhusu mzozo DRC

NA MWANDISHI WETU

KATIKA jitihada za kurejesha amani na utulivu mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), viongozi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) wamekutana katika Mkutano wa pamoja na kutoa mapendekezo na maamuzi muhimu kwa pande zote zinazohusika na mgogoro huo. Mkutano huo umeonesha mshikamano wa mataifa ya Ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika katika kusaka suluhisho la kudumu kwa mzozo ambao umeathiri maelfu ya raia wasiokuwa na hatia, huku wakitoa mapendekezo na maazimio kwa lengo kutoa suluhisho la mzozo huo.

Mapendekezo muhimu:

Usitishaji wa mapigano mara moja bila masharti yoyote:

Viongozi wa EAC na SADC wametaka kila upande unaohusika katika mgogoro wa DRC kusitisha mgogoro mara moja ili kuzuia madhara zaidi kwa raia na kuimarisha mazingira ya mazungumzo ya amani.

Ufunguzi wa Uwanja wa Ndege wa Goma:

Kufungwa kwa uwanja huo kumetatiza misaada ya kibinadamu na usafirishaji wa bidhaa muhimu. Mkutano huo umeagiza kufunguliwa mara moja kwa uwanja huo ili kuwezesha shughuli za kiuchumi na utoaji wa misaada kwa wahanga wa mgogoro huo.

Urejeshaji wa miili ya marehemu na uokoaji wa majeruhi:

Mkutano umeagiza urejeshaji wa miili ya wale waliopoteza maisha kutokana na mapigano pamoja na kuweka utaratibu wa haraka wa kuwahudumia majeruhi.

Mazungumzo jumuishi kwa ajili ya suluhisho la kudumu:

Pande zote zimetakiwa kushiriki kwenye mazungumzo ya wazi na jumuishi, yakizingatia mchakato wa Nairobi na Luanda, ili kupata suluhu la kudumu kwa mgogoro wa DRC.

Kutokomeza vikundi vya waasi na kuondoa majeshi ya Rwanda:


Mkutano umehimiza hatua za haraka za kuangamiza vikundi vya waasi kama FDLR na kutaka kuondolewa kwa majeshi ya Rwanda katika ardhi ya DRC.

Kufunguliwa kwa njia kuu za usambazaji wa bidhaa:

Ili kupunguza athari za kiuchumi kwa raia, viongozi wameamuru kufunguliwa kwa barabara kuu za usafirishaji wa bidhaa na misaada ya kibinadamu, ikiwemo njia zinazounganisha GomañSakeñBukavu, GomañKibumba, Rutshuru, Bunagana, na safari za majini katika Ziwa Kivu kati ya Goma na Bukavu.

Kukomesha hotuba za chuki:

Viongozi wamezitaka pande zinazohusika na mgogoro kuepuka hotuba zinazochochea chuki na badala yake kujikita katika mazungumzo yenye lengo la kujenga amani ya kudumu.



# TANZANIA INAENDELEA KUVUNA MATUNDA YA MKUTANO WA NISHATI

NA MWANDISHI WETU

KUNA kila dalili kuwa Tanzania itaendelea kufaidika kufuatia kufanyika Mkutano wa Nishati kwa nchi zaAfrika, uliomalizika juzi ukihusisha Wakuu wa nchi mbalimbali za Afrika, Mawaziri wa Kisekta, viongozi mbalimbali na wadau wa Maendeleo.

Neema inayoonekana kuangukia ardhi ya Tanzania ni utalii, ambao ulikuwa kivutio katika mkutano huo licha ya kutokuwepo katika Ajenga zenyewe.

Muda mfupi ambao Tanzania ilipata kuwaonyesha wageni hao, masuala ya utalii umetosha kuwashawishi wengi kati yao kutamani kurudi tena na hata kuwa mabalozi wa utalii katika nchi zao.

Tanzania ilikuwa katika kipindi cha kihistoria, ikishuhudiwa mkutano mkubwa uliojumuisha idadi kubwa ya wakuu wa nchi ukifanyikakatika ardhi ya Tanzania.



Baadhi ya wageni waliokuwepo katika mkutano huo ni kutoka nchi za Algeria, Comoro, Liberia, Lesotho, Botswana, Kenya, Ghana, Gabon, Sierra Leone, Ethiopia, Sudan, Malawi, Zambia, Somalia, Guine Bisau, Burundi, Mauritania, Kongo Brazzaville, Madagascar, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Libya, Nigeria, Djibouti na Gabon.

Ilikuwa wakati mzuri baada ya Tanzania kukaribisha nchini wadau wa maendeleo akiwepo Rais wa Benki ya Afrika (AfDB), Dkt. Akinumwi Adesina ambaye ameipongeza nchi ya Tanzania kwa kuwa mfano wa kuigwa kwa kufanya vizuri katika uwekezaji wa miundombinu ya umeme kwa kuwafikishia nishati ya umeme wananchi katika vijijini vyote 12,318.

Mkutano ule uliowakutanisha Mawaziri wa Nishati, Viongozi wa Taasisi za Kimataifa za Kifedha, Wataalam na Wadau wa Mashirika ya Kiraia ambao walipata fursa ya kujadili na kukubaliana malengo, vipaumbele vya sera vikawa ni suluhisho, na ahadi ya jinsi ya kutekeleza Mpango wa Mission 300.

Kuhusu kuvutika na utalii gazeti hili lipata nafasi ya kuzungumza na wajumbe kutoka mataifa mbalimbali ambao walieleza kuvutiwa na utalii wa Tanzania hasa, Hifadhi zake na hata kisiwa cha Zanzibar ambacho kwa siku za hivi karibuni chini ya Rais wa Awamu ya Nane Dkt Hussein Mwinyi kimekuwa kimbilio kwawatalii kutoka nchi mbalimbali duniani.

Hii ni fursa inayoendelea kuiitangaza Tanzania kimataifa, huku juhudi za Rais wa Awamu ya Sita Dk Samia Suluhu Hassan akistahili kupongezwa kwa juhudi zake za kurudisha mahusiano ya kimataifa ili kuifanya nchi iondoke katika hali tengefu kama kisiwa.


## TANGAZA NASI SASA

*Unatamani kukuza biashara yako kutoka hapo ilipo kuwa kubwa na yenye mantiki zaidi?*

- *Unatamani kuongeza kipato, uelewa na upana wa shughuli zako za kila siku?*
- *Je unataka kuwafikia wateja wako ndani na nje ya nchi kwa kiasi kikubwa ili kukuza biashara na huduma yako?*
- *Fahamu kwamba JAMVI LA HABARI na mitandao yake ya kijamii kama Youtube, Instagram, Facebook, Website na Twitter hutembelewa na maelfu ya wasomaji kila siku Duniani kote.*
- *Hivi unafahamu kuwa JAMVILAHABARI kwa sasa ni moja kati ya Media chache zinazo ongoza kwa kutoa taarifa sahihi na kwa wakati zinazotokea nchini na Duniani kwa ujumla?*

*TANGAZA SASA NA JAMVI LA HABARI KWA PUNGUZO KUBWA LA BEI UPATE MATOKEO YA HARAKA.*

*Kwa matangazo yote kama vile minada, kupotelewa kwa vyeti vya shule, matangazo ya makampuni, nafasi za kazi, zabuni za kazi, maonyesho, dawa za asili, taasisi za elimu, taasisi za dini na mengine mbalimbali mbali mbali.*

*Ni rahisi sana, wasiliana nasi kupitia Whatsap namba +255659555744 au tupigie katika +255743777778 au +255659555744 GHARAMA ZETU NISAWA NA BUREE JAMVILAHABARI; TUMECHAGUA KUKUHUDUMIA www.jamvilahabari.co.tz*

# Malawi kuondoa Jeshi lake DRC

NA MWANDISHI WETU

RAIS wa Malawi, Lazarus Chakwera, amemuagiza Kamanda wa Jeshi la nchi hiyo kujiandaa kuondoa majeshi ya Malawi kutoka eneo la mashariki nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

Taarifa iliyotolewa na serikali ya nchi hiyo imesema, uamuzi wa Rais Chakwera unalenga kuheshimu tangazo la kusitishwa kwa mapigano kati ya pande hasimu lilitolewa na waasi wa M23, ambao walifanya mashambulizi katika mji wa Nyabibwe katika Jimbo la Kivu Kusini, DRC.

Kuondolewa kwa wanajeshi wa Malawi kutatoa fursa ya kuendeleza mazungumzo ya kuelekea amani ya kudumu.

Rais Chakwera amekumbana na shinikizo kubwa la kimataifa kuhusu uamuzi wa kuondoa majeshi ya Malawi Mashariki mwa DRC, hasa baada ya wanajeshi watatu wa Malawi kuuawa katika mashambulizi ya M23 mjini Goma.

Maazimio muhimu:

Mkutano umeelekeza wakuu wa majeshi wa EAC na SADC kukutana ndani ya siku tano ili kutoa mwelekeo wa kina kuhusu usitishaji wa vita, utoaji wa misaada ya kibinadamu, na kuhakikisha usalama katika mji wa Goma na maeneo jirani.

Serikali ya DRC imetakiwa kuhakikisha ulinzi wa balozi na ofisi za kidiplomasia zilizoko Kinshasa kutokana na kuongezeka kwa mashambulizi dhidi ya ofisi hizo.

Pia, mataifa ya EAC na SADC yametakiwa kuendelea kushirikiana kidiplomasia na kisiasa ili kupata suluhu ya kudumu kwa mgogoro huo, badala ya kutegemea tu suluhisho la kijeshi.

# Msisitizo wa Dk Nchimbi kuhusu maadilili ndiyo dira ya maendeleo

NA MWANDISHI WETU

WANA CCM wanatakiwa kuhakikisha wanafuata maadili ya Chama ili kuendelea kueminika kama sifa ya Chama cha ambacho kimeridhiwa na Watanzamnia kutawala nchi tangu kilipoasisiwa mwaka 1977, na pia nyuma yake enei ya utawala wa Chama Cha TANU kilicholeta uhuru wa nchi hii

Hivi karibuni Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na Mgombea Mwenza wa Urais Tanzania Bara, Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi, amewahimiza wanachama wa Jumuiya ya Umoja wa Wazazi kuendelea kujipanga vyema ili kuhakikisha chama kinashinda kwa kuzingatia sera na maadili.

Ilikuwa ni katika kikao cha Kamati ya Utekelezaji ya Jumuiya hiyo jijini Dodoma, Dkt. Nchimbi alisisitiza kuwa CCM ni chama kinachojikita katika sera na maendeleo, si katika matusi au kejeli.

"Chama chetu kimefanya mambo makubwa kwa maendeleo ya taifa. Tunapaswa kuendelea kusimamia hoja zenye mashiko na si kutumia lugha zisizofaa. Tunapaswa kuwa mfano wa kuheshimu watu na kuzungumzia maendeleo yanayoonekana," alisema.

Aidha, alieleza kuwa serikali inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanikisha mambo mengi ambayo yanaweza kuwahamasisha wananchi kuendelea kukiamini chama.

"Tunayo mengi ya kuwaambia Watanzania kuhusu maendeleo yaliyofikiwa, hatuna sababu ya kutumia lugha za kejeli. Hayo tuwaachie wale wasiokuwa na hoja za msingi," aliongeza.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Wazazi Taifa, Fadhili Maganya, alisema kuwa ujio wa Dkt. Nchimbi katika kikao hicho ni ishara ya heshima kwao.

"Uwepo wako hapa umetupa faraja kubwa. Tumekukaribisha ili usikilize mawazo yetu na kutushauri. Hii ni historia, kwani sisi ndiyo jumuiya ya kwanza kuketi na wewe tangu uteuliwe kuwa mgombea mwenza," alisema Maganya.

Kikao hicho kilitoa fursa kwa viongozi wa Umoja wa Wazazi kujadili masuala muhimu yanayohusu ustawi wa jumuiya na mchango wake katika mustakabali wa chama kuelekea uchaguzi ujao.

Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi aliyasema haya kwenye Kikao cha Kamati ya Utekelezaji ya Baraza Kuu la Umoja wa Wazazi, Jumuiya ya CCM, ambacho alialikwa na kushiriki akiwa mgeni maalum, leo Jumamosi tarehe 8 Februari 2025, katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete, jijini Dodoma.



# Tanzania yazihakikishia EAC, SADC ushirikiano suluhu DR Congo

NA MWANDISHI WETU

RAIS Samia Suluhu Hassan amewahakikishia Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kuwa Tanzania itaendelea kutoa ushirikiano katika kushughulikia mgogoro unaoendelea Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (DRC).

Aidha, Rais Samia ametoa rai kwa Jumuiya hizo mbili kuchukua hatua kuhakikisha kuwa DRC, ambayo ni mwanachama wa EAC na SADC, inakuwa salama na mgogoro unaoendelea nchini humo unamalizika.

Kwa mujibu wa taarifa ya Ikulu Rais Dk Samia ameyasema hayo leo wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa pamoja wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa EAC na SADC uliofanyika katika Ikulu ya Dar es Salaam ili kujadili hali ya usalama Mashariki mwa DRC.

Rais Samia ameeleza kuwa hali inayoshuhudiwa Mashariki mwa DRC haikubaliki na ipo haja ya kuchukua hatua za haraka kumaliza mgogoro huo unaoleta mateso kwa wananchi.

Aamesema ana imani kuwa Mkutano huo utatoka na maazimio ambayo yatawezesha wananchi wa Mashariki mwa DRC kuishi amani.

Kwa upande wake Rais wa Jamhuri ya Kenya, ambaye pia ni Mwenyekiti wa EAC, Dk William Samoei Ruto amesema mgogoro unaoendelea Mashariki mwa DRC hautamalizwa kwa kutumia silaha bali kwa njia za kidiplomasia kupitia mazungumzo, kusikilizana na kushauriana.

Aidha, amewataka wadau wote kushirikiana na EAC na SADC ili kumaliza mgogoro huo ambao unaendelea kugharimu maisha ya wananchi wasio na hatia.

Kwa upande wake Rais wa Jamhuri ya Zimbabwe na Mwenyekiti wa SADC, Dk Emmerson Dambudzo Mnangagwa amesema hali inayoendelea Mashariki mwa DRC inaathiri bara zima la Afrika, hivyo nchi za Afrika zinapaswa kushikamana kama zilivyoshikamana wakati wa kupigania uhuru wa bara la Afrika.

# TAHARIRI

## Kwa hili CCM inastahili pongezi

WANACHAMA wa Chama Mapinduzi (CCM), sambamba na wananchi wote Tanzania wametakiwa kuwa makini na viongozi wenye tabia ya uchonganishi kwa kile walichodai baadhi yao kuchochea chuki inayoweza kuwatenganisha.

Hiyo ni kauli makini iliyotolewa na katibu wa NEC Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM Taifa ndugu Amos Makalla wakati akizungumza na Wananchi na wanachama wa Chama cha Mapinduzi katika Viwanja vya Umoja ni nguvu kusini Pemba ikiwa ni muendelezo wa ziara yake ya Mikoa 6 Visiwani Zanzibar.

Makalla pia amesema kuwa Dkt Samia Suluhu Hassan na Dkt Hussein Mwinyi hawana ubaguzi wowote kwenye suala la kuwaletea maendeleo lakini wenzetu kila kukicha wanaweka fitina na hili kazi kwenu Wazinzabar kwa ujumla wakataeni Viongozi hao na wanasiasa hao kwa kuwanyima kura wakati Uchaguzi utakapofika na tuchague chama cha mapinduzi ambacho ndio kina wajibu wa kuyaleta.

Kauli hii haistahili kupita bila kupongezwa ndiyo maama sisi JAMVI LA HABARI tunaipongeza kwa vile imezingatia kuleta umoja mshikamano na maelewano baina ya Watanzania.

Tunasema hayo tukijua kwamba kipindi kijacho yani Mwezi Oktona nchi itaingia katika kinyang'anyiro cha Uchaguzi Mkuu wa Rais, wabunge na Madiwani hivyo wasioitakia mema nchi wanaweza kutumia nafasi hiyo kuingiza chuki na hasama baina ya wananchi.

Tunaamini kila aliyesikia rai hii iliyotolewa na chama tawala, atazingatia kwa vile nchi hii ina wanasiasa na wasio wanasiasa ambao wanahitaji amani na utulivu.


## BODI YA UHARIRI

Mhariri Mkuu - 0762 178 678
Idara Ya Matangazo/Masoko - 0743 777 778, - 0659 555 744
Idara Ya Usambazaji - 0676807684, - 0787 288 160

Gazeti hili hutolewa na **JAMVI MEDIA GROUP**
S. L. P 78862, Dar es Salaam
**Tel:** +255 676 807684, 255 743 777778
**Email:** jamvinews@gmail.com
www.jamvilahabari.co.tz




*Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi akizungumza kwenye Kikao cha Kamati ya Utekelezaji ya Baraza Kuu la Umoja wa Wazazi, Jumuiya ya CCM, ambacho alialikwa na kushiriki akiwa mgeni maalum, jana Jumamosi tarehe 8 Februari 2025, katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete, jijini Dodoma.*

UCHAMBUZI

# Ushindi wa CCM unatokana na utekelezaji wa ilani yake

NA MWANDISHI WETU

SIRI kubwa ya maandalizi ya CCM Kushinda uchaguzi Mkuu na kuendelea kushika Doila, ni utekelezaji wa Ilani ya chama hicho ambayo viongozi, waliopewa nafasi walibeba na kuifanyia kazi kila eneo.

Hilo ndilo linaloweza kuwafanya wagombea wa chama hicho akiwemo mgombea nafasi ya Urais Dkt Samia Suluhu Hassan pamoja na jopo la wviongozi wengine watakaopambania nafasi za Ubunge na Madiwani.

Tayari chama hicho kimefanya chaguzi za ndani kama vile ule uliohusisha Mkutano Mkuu wa CCM, ulimchagua Mzee Steven wassira kuwa Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Bara.

Wassura aliyekuwa nje ya madaraka ya kisiasa kwa muda mrefu kwa maneno yake mwenyewe alieleza kushangazwa na ushindi ule na akaahidi kuifanya kazi hiyo kwa uadilifu na unyenyekevu mkubwa, kama hatua ya kulipa fadhjila na heshima ile kubwa.

Pia mkongwe huyo akatabiri ushindi wa kishindo utakaokipata chama chake, mtaji mkubwa ukiwa ni utekelezaji wa Ilani na jinsi chama hicho kinavyoendesha siasa zake kwa njia ya uwazi na uwajibikaji.

Mkongwe huyo ameingia na Falsafa ya Umoja Maridhiano na Ushindi, kazi ambayo amewaahidi wajumbe waliomuamini kushika wadhifa huo kuwa ataifanya kwa bidii kubwa huku akiamini ni jukumu lenye baraka za Mungu.

Kwa tathmini nyepesi ya ushindi huu wa Wasira una maana kubwa kwa CCM kuekelea uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani utakaofanyika mwaka huu, mwezi Okttoba kwamba mtaji wake unaonekana umeongezeka

Ukichukulia kuwa CCM ndicho chama kinachoongoza nchini kwa kuwa na wanachama na wapenzi wengi kinaweza kutumia mtaji huo kumpa ushindi wa kishindo mgombea wake wa Urais na hata Wabunge na Madiwani.

CCM ina watu wengi hata isipohitaji kura ya wapinzani au watu wasiofungamana na siasa ya chama chochote bado wana uhakika wa kushinda hususa nafasi ya Urais pengine baadhi ya wabunge wachache wanaweza kupoteza viti kutokana na kutowafanyia vizuri wapiga kura wao katika kipindi kilichopita.

Mgombea wa CCM anasaidiwa na maendeleo yanayoonekana kila kona, atahitaji timu ya kawaida tu kumnadi na kuweza kumpa ushindi wa kimbunga kama huu alioanza kuonyesha dalili Mzee Wasira

Ushindi wa CCM mwaka huu unaonekana bila kuhitaji utafiti mkubwa, kwani hata ukiangalia upande wa upinzani bado unaonekana kama hakuna chama chenye nguvu kama ilivyokuwa katika chaguzi za awamu zilizoipita tangu kuanzishwa mfumo wa vyama vingi vya Siasa mwaka 1992

Licha ya CCM kujiandaa kama ilivyokuwa wakati wote inapoingia katika uchaguzi, lakini mwaka huu licha ya uwepo wa maridhiano ya kisiasa, lakini upinzani unaonekana kupoteza nguvu kuliko miaka yote ya uchaguzi.

Ni mwaka tutakaoendelea kusikia vishindo vya CCM katika majimbo na makelele ya wapinzani watakaoendeleza msamiati wa kuibiwa kura ili hali hawakuwa na maandalizi zaidi ya malumbano na kukashifiana.

# Matarajio ya viongozi wa EAC na SADC

NA MWANDISHI WETU

KATIKA jitihada za kurejesha amani na utulivu mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), viongozi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) wamekutana katika Mkutano wa pamoja na kutoa mapendekezo na maamuzi muhimu kwa pande zote zinazohusika na mgogoro huo.

Mkutano huo umeonesha mshikamano wa mataifa ya Ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika katika kusaka suluhisho la kudumu kwa mzozo ambao umeathiri maelfu ya raia wasiokuwa na hatia, huku wakitoa mapendekezo na maazimio kwa lengo kutoa suluhisho la mzozo huo.



Mapendekezo muhimu:

Usitishaji wa mapigano mara moja bila masharti yoyote:

Viongozi wa EAC na SADC wametaka kila upande unaohusika katika mgogoro wa DRC kusitisha mgogoro mara moja ili kuzuia madhara zaidi kwa raia na kuimarisha mazingira ya mazungumzo ya amani.

Ufunguzi wa Uwanja wa Ndege wa Goma:

Kufungwa kwa uwanja huo kumetatiza misaada ya kibinadamu na usafirishaji wa bidhaa muhimu. Mkutano huo umeagiza kufunguliwa mara moja kwa uwanja huo ili kuwezesha shughuli za kiuchumi na utoaji wa misaada kwa wahanga wa mgogoro huo.

Urejeshaji wa miili ya marehemu na uokoaji wa majeruhi:

Mkutano umeagiza urejeshaji wa miili ya wale walipoteza maisha kutokana na mapigano pamoja na kuweka utaratibu wa haraka wa kuwahudumia majeruhi.

Mazungumzo jumuishi kwa ajili ya suluhisho la kudumu:

Pande zote zimetakiwa kushiriki kwenye mazungumzo ya wazi na jumuishi, yakizingatia mchakato wa Nairobi na Luanda, ili kupata suluhu la kudumu kwa mgogoro wa DRC.

Kutokomeza vikundi vya waasi na kuondoa majeshi ya Rwanda:

Mkutano umehimiza hatua za haraka za kuangamiza vikundi vya waasi kama FDLR na kutaka kuondolewa kwa majeshi ya Rwanda katika ardhi ya DRC.

Kufunguliwa kwa njia kuu za usambazaji wa bidhaa:

Ili kupunguza athari za kiuchumi kwa raia, viongozi wameamuru kufunguliwa kwa barabara kuu za usafirishaji wa bidhaa na misaada ya kibinadamu, ikiwemo njia zinazounganisha GomañSakeñBukavu, GomañKibumba, Rutshuru, Bunagana, na safari za majini katika Ziwa Kivu kati ya Goma na Bukavu.

Kukomesha hotuba za chuki:

Viongozi wamezitaka pande zinazohusika na mgogoro kuepuka hotuba zinazochochea chuki na badala yake kujikita katika mazungumzo yenye lengo la kujenga amani ya kudumu.

Mashambulizi ya M23 ma majeshi ya Serikali ya DRC yalikuja kwa nguvu na kutishia ukanda huo, huku Video nyingi za mauaji na vitisho vya milio ya silaha nzito zilizosambaa kila kona na kuzua hofu kwa wananchi wa nchi ya Kongo pamoja na ndugu na jamaa wa nchi mbalimbali waliokuwa na ndugu zao huko.

Hata hiyo baadya kwa upande wa Tanzania zikasikika taarifa za kuokolewa baadhi ya Watanzania katika eneo hilo la Goma yalipokuwepo majeshi ya nchi mbalimbali za Afrika Mashariki wakisaidiwa na yale ya MUNUSCO, ambayo yaliendekea kukabiliana na upinzani kutoka kundi
Waasi wa M23.

Wakati majeshi hayo ya
iendelea kupambana ili kut
liza amani, kuliibuka vu
gu nyingine mitaani kati
miji mbalimbali ya DRC a
bapo waandamanaji wana
inga kuendelea kuwepo k
majeshi ya MUNUSCO.

Walishinikiza kutoka
taji uwepo wa majeshi ha
huku wakiendesha viten
vya uporaji pamoja na k
choma moto baadhi ya bal
ya nchi wanaotoka wanajes

# C kurejesha amani Goma yanatia moyo



> Mkutano umeagiza urejeshaji wa miili ya wale waliopoteza maisha kutokana na mapigano pamoja na kuweka utaratibu wa haraka wa kuwahudumia majeruhi.

la
ak-
tu-
ru-
ka
m-
p-
wa
hi-
yo
do
u-
izi
shi

wanaounda jeshi hilo.

Katika hatua nyingine Wafanyakazi wawili katika ubalozi wa Kenya katika mji mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo Kinshasa, walilazimika kutoroka na kutafuta hifadhi kwingine huku waandamanaji wakilenga jengo hilo mapema leo, serikali ya Kenya imesema.

Umati wa watu wenye hasira wakilalamikia shambulio la waasi dhidi ya Goma pia walishambulia balozi za Rwanda, Uganda, Ufaransa na Ubelgiji, wakidai kutowahitaji kuoina Askari wa MUNUSCO.

Katika taarifa yake, wizara ya mambo ya nje ya Kenya ilisema inasikitishwa sana na mashambulizi hayo ikiyataja kuwa "hayafai" kukaliwa kimya.

Iliongeza kuwa kumekuwa na uporaji, na uharibifu wa mali unaoendelea kudumu kila uchao huku ikisababisha madhila makubwa kwa wananchi wa maeneo hayo wakiwemo wanawake na watoto.

Taarifa hiyo ilidai kuwa wakati shambulio dhidi ya ubalozi huo lilitokea "mchana" huku maafisa wa usalama wa Congo wakishuhudia na, "hawakuchukua hatua yoyote kuzuia hali hiyo".Ilielezea kile kilichotokea kama ukiukaji wa sheria.






# BWAWA LA MWALIMU NYERERE TUMAINI LA UMEMA AFRIKA



NA MWANDISHI WETU

HIVI Karibuni Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, alikaririwa na vyombo vya habari akisema kuwa mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Julius Nyerere utakamilika rasmi mwishoni mwa Februari, mwaka huu, baada ya kukabidhiwa mtambo wa tisa wa kuzalisha umeme.

Aalikuwa akichangia Bungeni azimio la kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kutokana na kuwa mwenyeji wa mkutano wa kimataifa wa nishati Afrika, Dk. Biteko alisema bwawa hilo lilipaswa kukamilika ifikapo Mei mwaka huu.

Siku hiyo kulifanyika tukio kubwa katika eneo hilo la mradi naye akawaeleza Wabunge kuwa, “Hadi leo asubuhi mitambo yote minane imekabidhiwa na mtambo mmoja, ambao ni wa tisa, utakabidhiwa mwishoni mwa Februari, mwaka huu, na mradi wa bwawa hili tutakuwa tumemaliza,î alisema.

> “Biteko alisema mkutano huo ulikuwa na mwitikio mkubwa wa watu kutoka mataifa mbalimbali ya Afrika kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na Rais Samia.

Siku hiyo akaongeza kuwa, mpango huo wa nishati umetoa viashiria vitano kikiwamo cha upatikanaji wa umeme kwa Tanzania kwa asilimia 78.4.

Aliongeza kuwa katika mpango huo walitia saini miaka mitano ijayo Tanzania itafikia upatikanaji wa umeme kwa asilimia 100.

ìUunganishaji umeme na wateja leo tunapozungumza hatua tuliyo nayo, tumeunganisha wateja milioni 5.5 na mpango ni kupeleka kwa wateja milioni 13.5 na usingekuwa mpango huo wangepambana na wasingezidi milioni 5.2,î alisema.

Alisema kuwa kwenye nishati safi ya kupikia wanataka watoke asilimia 9.9 kwenda asilimia 75 ndani ya miaka mitano.

ìMchango wa nishati jadidifu itoke asilimia 56 iliyopo twende asilimia 65 na tutalifikia suala hili bila wasiwasi wowote,î alisema.

Biteko alisema mkutano huo ulikuwa na mwitikio mkubwa wa watu kutoka mataifa mbalimbali ya Afrika kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na Rais Samia.

ìSababu mbili zilizofanya mkutano huu kuja Tanzania ni kuimarika kwa diplomasia yetu na mataifa mengine na haijaimarishwa na mwingine ni yeye Rais Samia. Kasi kubwa ya upelekaji umeme kwa wananchi hasa vijijini, Benki ya Dunia walivyofanya tathmini mwaka jana Tanzania iliongoza na wakaona mahali pekee pakupeleka mpango huu ni Tanzania,î alisema.

Alibainisha kuwa Rais Samia ametoa msukumo mkubwa kwenye sekta ya nishati na kuahidi makubaliano yaliyofikiwa kwenye mkutano huo atayasimamia na hayatabaki kwenye makaratasi.

Naye Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alipongeza serikali kwa kukamilisha mradi wa Nyerere kabla ya muda uliopangwa na kwamba fedha zilizokuwa zinaelekezwa kwenye masuala ya umeme sasa zitapelekwa miradi mingine ikiwamo barabara ambazo wabunge wamekuwa wakipigia kelele.

Amezitaja wilaya zitakazonufaika kuwa ni pamoja na Wilaya ya Rombo, Hai, Same, Moshi, Mwanga na Siha .ya kupikia 3,255 kusambazwa Kila wilaya.



# MBINU MPYA ZA KIBIASHARA TANZANIA

NA MWANDISHI WETU

KUNA fikra potofu zimejengeka miongoni mwa watu wakidhani kuwa kufanya kazi kwa bidii ni utumwa. Hii ni kutokana na dunia ya sasa kujaa watu wasiopenda kazi na wavivu.

1. Bidii inasaidia Kutumia Muda Vyema

Huwezi kutumia muda vyema kama hutofanya kazi kwa bidii. Ukiwa na bidii katika kufanya kazi, unaweza kufanya kazi za siku nzima ndani ya saa moja au kazi za siku mbili ndani ya siku moja.

Hakuna mtu yeyote aliyefanikiwa bila kutumia muda vyema; muda ni mali, hivyo yakupasa uutumie vyema kwa kufanya kazi kwa bidii.

2. Bidii inasaidia Kufikia Malengo Yako

Kanuni moja wapo ya kufikia malengo ni kufanya kazi kwa bidii. Safari ya mafanikio siyo ya mteremko, inahitaji juhudi nyingi ili tuweze kuona matokeo.

Hakuna mtu aliyewahi kufanikiwa kwa kufanya kazi kivivu; fuatilia watu waliofanikiwa watakueleza jinsi wanavyofanya kazi usiku na mchana ili kukamilisha ndoto zao.

3. Bidii inasaidia Kuheshimika

Nani atamheshimu mvivu? Kwa hakika hakuna. Mtu anapokuwa mwenye bidii utasikia kauli kama vile huyo hapendi mchezo, akishaingia kwenye kazi zake humpati, hageukagi nyuma kwenye kazi huyo, kama huyo yupo hiyo kazi lazima iishe, n.k.

Hizi ni baadhi ya kauli zinazoonyesha kuheshimiwa kwa mtu husika kutokana na kufanya kazi kwa bidii. Ikiwa unataka kuheshimika ni lazima ufanye kazi kwa bidii.

4. Bidii inasaidia Kutambulika

Ikiwa unafanya kazi kwa bidii huna haja ya kujikombakomba kwa wakubwa au mbele za watu ili utambulike; bidii yako ya kazi itakutambulisha.

Naamini umewahi kusikia watu wakipewa tuzo kwenye sherehe za kitaifa kutokana na kufanya kazi kwa bidii; hili linatupa picha ya kipekee ya faida ya kufanya kazi kwabidii.

Usijali hata kama wanakudharau au wanakuona duni, wewe fanya kazi kwa bidii watakutambua ukiwepo au hata wakati utakapoondoka wataona pengo lako.

5. Bidii inasaidia Kuondoa Lawama

Mara nyingi idara au ofisi zenye malalamiko mengi ni zile zenye wafanyakazi wavivu. Pia wafanyakazi wengi wanaolaumiwa na kunyoshewa vidole na waajiri wao, wengi ni wale wavivu.

Ili kuepuka lawama au manungíuniko, ni vyema ukafanya kile unachokifanya kwa bidii kwani kwa njia hii utaongeza ufanisi wako.

6. Bidii inasaidia Kupata Matokeo Makubwa

Hakuna matokeo makubwa bila kazi kubwa, yaani kazi iliyofanywa kwa bidii. Kwa mtu yeyote anayetaka kuona matokeo makubwa katika kile anachokifanya ni lazima kwanza afanye bidii.

Kumbuka hata mkulima anayefanya bidii katika kilimo ndiye huvuna zaidi ya wakulima wengine. Hivyo kufanya kazi kwa bidii hakuepukiki kwenye maisha.

7. Bidii inasaidia Huleta Fursa Mpya

Mtu mwenye bidii kila mara hufungua milango ya kupata fursa mpya, kazi zake na bidii yake humtangaza na kumfungulia fursa zaidi. Hakuna mtu atakayempa mtu mvivu kazi au fursa zenye manufaa.

8. Bidii inasaidia Kuboresha Afya

Kukaa bila kufanya kazi ni kujiletea matatizo ya kiafya; kazi ni sehemu ya mazoezi. Hivyo kufanya kazi kwa bidii kutakufanya uwe mwenye afya njema kila wakati.

Unalotakiwa kukumbuka hapa ni kuwa na kiasi, fanya kazi kwa bidii lakini usipitilize hadi uathiri afya yako.



# KAMPENI YA UIBUAJI WA WAGONJWA WA KIFUA KIKUU

NA MUHIDIN AMRI, TUNDURU

WIZARA ya Afya kupitia mpango wa Taifa wa kudhibiti Kifua Ki kuu na Ukoma imesema, kampeni ya mpango harakishi wa uibuaji Wagonjwa wa Kifua Kiku u itawafikia watu wote walioba inika kuwa na maambukizi ya ugonjwa huo ambao hawakufikiwa mwaka 2024.

Watu hao, wataanzishiwa Dawa ha raka kwa ajili ya kuzuia uweze kano wa kuambukiza watu wengin e ili kuifanya Tanzania kuwa nchi salama bila kuwa na watu walioambukizwa ugonjwa wa kifua kikuu ifikapo mwaka 2 030.

Hayo yamesemwa jana na Mwakili shi wa Wizara ya Afya kitengo cha kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma Dkt Jacob Mwanamtwa, baada ya kukagua utekelezaji wa kampeni hiyo katika maeneo mbalimbali ya wilaya ya Tunduru Mkoani Ruvuma.

Alisema, Wizara ya Afya imejipa nga na itahakikisha inawapata wagonjwa ambao hawakupatikana mwaka 2024 na kuwaanzishia matibabu yanayotolewa bure kwenye vituo vya Afya na Hospitali zote hapa nchini.

"Wagonjwa ambao hawajapatiwa m atibabu wanaendelea kuambukiza watu wengine katika jamii yetu na mbaya zaidi mgonjwa ambaye hajaanza kutumia Dawa anaweza kuambukiza watu kati ya 10 hadi 15 kwa mwaka" alisema Dkt Jacob.

Alisema, wameanza kampeni hiyo kwenye mikoa tisa hapa nchini ambayo haikufanya vizuri katika kuibua wagonjwa wa kifua kikuu mwaka jana ikiwemo Mkoa wa Ruvuma na kupitia kampeni hiyo wagonjwa wote watafikiwa ili waweze kuanzish iwa matibabu.

Alisema, malengo ya Shirika la Afya Duniani(WHO) kutokomeza ugonjwa huo ifikapo mwaka 2030 , lakini kutokana na changamoto mbalimbali yanaweza yasifikiwe au yakafanikiwa kutokana na mikakati iliyowekwa na Serikali yetu kupitia Wizara ya Afya.

Mratibu wa Kifua Kikuu na Ukom a wa Wilaya ya Tunduru Dkt Mkasange Kihongole alisema, kupitia kampeni ya mpango harakishi watahakikisha wananchi wote wanapata elimu ya kifua kikuu, wanafanyiwa



***Muhudumu wa afya ngazi ya jami i Idd Yakiti(Nyuki) alisema, kwenye kampeni ya uibuaji wa Wagonjwa wa Kifua Kikuu kazi anayofanya ni kwenda kwenye zahanati ili kuchukua makohozi ya wahisiwa na kuzifikisha Hospitali ya wilay a kwa ajili ya uchunguzi.***

uchunguzi na ambao watabainika kuwa na vimelea vya ugonjwa huo wataanzishiwa dawa.

"katika kipindi hiki cha mpito ambacho tunatakiwa kufanya kazi kwa juhudi kubwa tumeanza kuangalia maeneo hatarishi zaidi, baada ya hapo wataalam tutasambaa kwenye maeneo mengine ambayo siyo hatarishi lakini kuna watu ambao wako kwenye hatari ya kupata ugonjwa huo"alisema Mkasange.

Mkasange ametaja maeneo hatari shi ni kwenye maboma ya wafuga ji, vijiwe vya boda boda, wachez a bao, Pooltable machimbo ya madini na maeneo mengine yenye mikusanyiko ya watu kuanzia watano na kuendelea.

Aidha alisema, kabla ya Wizara ya Afya kuzindua mpango haraki shi wa kuibua wagonjwa wa TB, Wilaya ya Tunduru imeshaanza kutekeleza kampeni hiyo kwenye vijiji vyote vinavyozun gukwa na machimbo ya madini, shule za Msingi na Sekondari za bweni.

Mkasange alisema, walianza kamp eni ya uelimishaji, uibuaji na uchunguzi wa TB mapema ili kwenda na kasi ya mpango harakishi wa uibuaji Wagonjwa wa Kifua Kikuu iliyozinduliwa wiki iliyopita ili kukata mnyororo wa maambukizi katika wilaya ya Tunduru.

Naye Mratibu wa huduma za maab ara Mkoa wa Ruvuma Said Kaunde alisema, kampeni ya mpango harakishi ya uibuaji Wagonjwa wa Kifua Kikuu imegawanyika kwenye makundi mawili ambayo ni kuwafikia Wananchi wenye vimelea vya TB kwa ajili ya kuchukua sampuli za makohozi na kuwaanzishia Dawa.

Alisema, katika mkakati wa kuto komeza ugonjwa huo Serikali yetu imewekeza fedha nyingi kwenye vifaa tiba hasa kununua mashine za kisasa za uchunguz i wa vimelea vya kifua kikuu na katika Mkoa wa Ruvuma kuna mashine 11 ambazo zimepelekwa kwenye Halmashauri zote nane.

Pia alisema, tangu kampeni hiyo ilipoanza hadi sasa wamefanik iwa kukusanya sampuli zaidi ya 851 ambazo baada ya kupelekwa maabara kwa ajili ya uchunguzi,24 zimekutwa na maambukizi ya ugonjwa huo.

Muhudumu wa afya ngazi ya jami i Idd Yakiti(Nyuki) alisema, kwenye kampeni ya uibuaji wa Wagonjwa wa Kifua Kikuu kazi anayofanya ni kwenda kwenye zahanati ili kuchukua makohozi ya wahisiwa na kuzifikisha Hospitali ya wilay a kwa ajili ya uchunguzi.

Nyuki, ameipongeza Serikali kup itia Wizara ya Afya kwa kuchuk ua hatua katika kukabiliana na ugonjwa huo ambao ni miongoni mwa magonjwa kumi Ulimwenguni yanayoongoza kusababisha vifo vya watu wengi.



# IJUE DRC; UTAJIRI WAKE UNAPOGEUKA SHUBIRI




NA MWANDISHI WETU

JAMHURI ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), imekumbwa na migogoro, vita na mapigano hasa Mashariki mwa nchi, kwa miongoni takribani mitatu.

DRC, idadi ya watu ni takribani 111,347,333 kwa mujibu wa tovuti inayofuatilia data mbalimbali duniani Worldometer.

Ukubwa wa eneo la ardhi DRC, linakadiriwa kuwa ni mara mbili ya nchi ya Tanzania. Upande wa Mashariki mwa DRC linajumuisha majimbo ya Ituri, Kivu kusini na Kivu Kaskazini yana jumla ya makundi ya wapiganaji zaidi ya 129.

Mchambuzi wa masuala ya kisiasa kitaifa na kimataifa, Dk. Richard Mbunda, akizungumza kwenye mahojiano na redio Clouds, wiki hii, ameielezea nchi hiyo, akiitaja kuwa na historia ya migogoro kwa miongo kadhaa. Anasema utajiri wa DRC, kuanzia uwapo wa ardhi yenye rutuba, madini ambayo mengi ni tegemeo la viwanda vikubwa duniani katika vifaa vya kiteknolojia, kumeisababishia migogoro.

ìMali zilizoko DRC zikitafsiriwa inaongoa kwenye orodha ya nchi tajiri duniani, ikishika namba mbili. Tafsiri ya nchi katika uchumi wake huangaliwa Pato la Taifa (GDP).

ìKwa sasa GDP ya Marekani ni dola trilioni 25, ikifuatiwa na China wana dola trilioni 17. Ila uatajiri Congo kama ukivunwa ni dola trilioni 24, ingekuwa ya pili duniani,î anasema.

Anasema mgororo wa nchini humo unachangiwa na vyanzo kadhaa; nchi majirani; makampuni ya uwekezaji ya kigeni; ubaguzi, sababu za kisiasa na wenyewe kwa wenyewe.

Kuhusu nchi majirani, anasema kuwa miongoni mwa sababu za mgogoro DRC, kunatokana na majirani zake kuwa na maslahi ya kiusalama, kwa kuwa nchi hiyo haina utulivu,

ìNchi majirani zilikuwa na maslahi ya kiusalama, wakati huo Zaire ya Mobutu (Sese Seko), ambayo ilikuwa inakumbatia vikundi vya waasi, likiwamo la FDLR.

Baadhi ya vikundi inasadikiwa Mobutu alivifadhili. Ila vingine vilitokana na ukosefu wa utengamao wa kisiasa nchi hiyo vikazaliwa vikundi vingine vingi,î anasema.

Kwa upande wa jirani yake Uganda, kiongozi Joseph Kony, aliongoza kiundi cha waasi Lords Resistance Army (LRA), walikuwa wanajipanga kwenda kumpindua Kagame.

Kwa hiyo Kagame naye akaona Congo inatunza kikundi cha waasi ambao wanaweza kuja kunipindua. Akawa na kikundi chake. Wote walijipanga wakiwa ndani ya DRC. Rwanda nayo ikawa inajilinda ikiwa ardhi ya DRC.

Angola, pia nao walikuwa wako Congo, walikuwa wanapata msaada na ushirikiano kutoka kwa Mobutu. Kwa hiyo aliwasaidia kuwaunganisha vikundi vya Rwanda, Uganda na Angola, kumsaidia.

Kilikuwapo kikundi kilichokuwa kinaungwa mkono na Rwanda, ëRarry for the Congolese Democracyí-RCD kiliongozwa na Ernest Wamba dia Wamba. Likaendelea kubadilika kulingana na wakati hadi kufikia kuwa M23.î

Anasema kipindi hicho miaka ya 1997 kilikuwapo vikundi vingi DRC kwa maslahi tofauti na vlikuwa vinaungwa mkono kutoka baadhi ya nchi zao.

FDLR, wanaodai wanajipanga kwenda Rwanda, bado wapo DRC. Baadae kundi ambalo lilikuwa linaungwa mkono na Rwanda, baadae likabadilika kuwa CNDP kama kundi la waasi na mwaka 2009 kulikuwa na makubaliano chini ya Joseph Kabila, Rais wa wakati huo DRC. CNDP wakabadilika kuwa chama cha siasa.

CNDP lilikuwa ni kundi la waasi lililoanzishwa na Laurent Nkunda katika eneo la Kivu katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Desemba 2006. CNDP ilihusika katika mzozo wa Kivu, mzozo wa silaha dhidi ya jeshi la Congo. Januari 2009, CNDP iligawanyika na Nkunda alikamatwa na serikali ya Rwanda na kikundi chake kilichogawanyika, kinachoongozwa na Bosco Ntaganda, kilipangwa kuunganishwa katika jeshi la taifa.

ìMalengo makubwa ya wao (CNDP) kuwa sehemu ya serikali hayakutimia, likaamua kujiondoa, wakaunda M23, kwa maslahi yao wenyewe kwa sababu wanajiangalia kama Wacongo, ingawa Wacongo wao wanaangalia kama watu wakuja. M23 hamu yao ni kuwa sehemu ya utawala wa Congo,î anafafanua.

Anasema maslahi mengine kwa nchi ya DRC yanatoka nje ya nchi, kutokana na uwapo wa makampuni yaliyowekeza hasa katika uchimbaji wa madini

UTAJIRI

Utajiri wa DRC, unaweza kuutaja uliobakia kwenye nadharia, licha ya kuwa ni nchi tajiri zaidi duniani kwa maliasili.

Ina madini mengi ghafi ambayo hayajatumika na yanadaiwa kuwa`na thamani ya hadi takriban dola trilioni 24.

Amana hizo ni pamoja na akiba kubwa zaidi ya madini ya coltan na kiasi kikubwa cha madini ya kobalti.

Hata hivyo kutokana na urahisi wa uchimbaji wa rasilimali hizo, taifa hilo utajiri wake wa madini hayo, umegeuka shubiri.

DRC ina maji yasiyo na kikomo, kutoka mto wa pili kwa ukubwa duniani, Congo, hali nzuri ya hewa na udongo wenye rutuba mbali na madini kama vile shaba, dhahabu, almasi, urani, koltani na mafuta ni baadhi tu ya madini ambayo yanapaswa kuifanya kuwa moja ya nchi tajiri zaidi duniani.

# Michezo Kimataifa

## Tetesi za soka



CHELSEA wanaamini wanaweza kufanya dili kwa ajili ya mlinzi wa Sporting Ousmane Diomande msimu wa joto - chini ya kipengele cha ukubwa wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast mwenye umri wa miaka 21. (TeamTalk),



JUVENTUS wameipa Chelsea ruksa ya kumsajili kiungo wa kati wa Brazil Douglas Luiz, 26, ambaye pia ananyatiwa na Manchester City na Arsenal, hii imetokana na mazungumzo mazuri kati ya klabu hizo na pia maslahi yaliyoridhiwa na pande hizi mbili.




1 MSHAMBULIZI wa Uingereza Harry Kane, 31, amekataa kuzungumza kuhusu ripoti kwamba anaweza kuhamia Arsenal mwaka ujao, kwa sababu ya kipengele cha kutolewa katika kandarasi yake ya Bayern Munich. (Mirror)

BAADA ya kulaulimiwa kwa muda mrefu kuwa tatizo la Arsenal ni kudharau kufaya usajili hasa eneo la ufungaji, hatimaye klabu hiyo imesikia kilio hicho na sasa imeanza mawindo makali ili kutibu pengo lililopo, kufutia mkakati huyo klabu hiyo imeingia chimbo na kumnasa Straika makali Raia Slovenia anayekipiga katika klabu ya RB Leipzig ya Ujerumani





## SIMBA YAKATAA OFA KWA KIBU DENIS

NA MWANDISHI WETU

BAADA YA kuikabili wenyeji wao Foutain Gate katika uwanja wa Tanzanite Kwaraa ulioko Babati mkoani Manyara, Wekundu wa Msimbazi wamekataa kumuuza nyota wao, Denis Kibu, kwa MC Algers ya Algeria, imefahamika.

Mechi huo ulikuwa wa tisa kwa Simba kushuka nje ya uwanja wake wa nyumbani, ambapo katika michezo nane imepata ushindi wa asilimia 100.

Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, aliliambia gazeti hili, timu yake imejipanga kuondoka na pointi tatu muhimu ili kuendeleza kutoa dozi katika kila inapocheza ugenini msimu huu.

Kocha huyo alisema Simba imekuwa na matokeo mazuri inapocheza ugenini na hii inachagizwa na idadi kubwa ya mashabiki wanaojitokeza viwanjani kuwashangilia wachezaji wao.

"Nilisema na narudia tena, tunashinda sana ugenini kwa sababu tunacheza mechi za mikoani kama tupo nyumbani kutokana na kushangiliwa na mashabiki wengi zaidi kuliko wapinzani wetu ambao ni wenyeji, natarajia mechi hii itakuwa hivyo hivyo, na sisi tutawapa na kuwaachia mashabiki furaha ya ushindi, tukichukua pointi tatu na kurejea nazo Dar es Salaam," alisema Fadlu.

Hata hivyo, Simba inaweza kumkosa winga wake tegemeo, Kibu, aliyeumia katika mchezo uliopita, ingawa daktari wa timu, Edwin Kagoba, amesema hali yake inaendelea vizuri.

"Yuko katika hatua ya pili ya matibabu, tunategemea, atakapopita kwenye hatua zote za matibabu anaweza kuwapo kwenye mchezo wetu ujao. Ila hii uwepo wake ni nusu kwa nusu, kuna vitu tunaviangalia leo (jana) na kesho (leo), lakini niwatoe hofu wanachama na mashabiki wa Simba hali yake si mbaya si ya kumweka nje muda mrefu," alisema daktari huyo.

Naye Kocha Mkuu wa Fountain Gate, raia wa Kenya, Robert Matano, amesema amekiandaa vyema kikosi chake kushindana na Simba, ingawa anaamini watawapa upinzani mkali.

# Burudani



# Mzee Nguza alirudisha Marquiz Og

NA HENRY PAUL

NYUMA ya mwaka 1978 bendi ya Orchestra Marquiz Dy Zaire ilikuwepo, kwani wanamuziki wake waliingia mapema tangu 1972 na kufanya mambo makubwa katika tasnia ya muziki wa dansi hapa nchini.

Iliburudisha kwa nyimbo zake na hata kutunga baadhi kwa ajili ya kuhamasisha maendeneo ya nchi ya Tanzania licha ya wanamuziki wengi waansilishi walitokea nchini Zaire sasa inatambulika kama DRC.

Ukisiiza albam iliyorekodiwa Tarehe 21.1.1977 iliyokuwa mamalum kwa ajili ya nyimbo mbili Azimio la Arusha na Chama kipya unanielewa kwa nini nimesisitiza kuwa bendi hii ilishiriki kwa kiasi kikubwa nyimbo za kuhamasisha maendeo ya kiuchumi, Siasa na Jamii.

Lakini pamoja na uwepo wa bendi hiyo na kufanya mambo makubwa lakini idadi kubwa ya mashabiki iliongezeka zaidi Mwaka 1977 wakati bendi hiyo ilipojiongeza kwa kubnoresha zaidi muziki wake ikiajiri wanamuziki wenye vipaji ili kushirikiana na wenzao kulisukuma mbele jahazi la bendi hiyo.

Miongoni mwawanamuziki hao ni pamoja na mwimbaji mwenye kipaji cha hali ya juu, Kikumbi Mwanza Mpango al maarufu King Kikii au Mzee wa Kitambaa Cheupe.

Pamoja naye pia aliongezwa mpiga Dram mkali aitwaye Mutombo Sozzy, pia Mpuliza Tarumbeta Kanku Kelly, Mcheza Shoo Ngalula Tshiandanda na Mpiga Ridhim besi Ilunga Kunga Banza Mchafu.

Ujio wa wanamuziki hawa uliongeza nguvu kwa magwiji wengine waliotangulia akiwemo aliyekuwa Rais wa bendi hiyo Chinyama Chiaza, Nguza Vicking Manyola (Kiongozi msaidizi), Ilunga Lubaba aliyekuwa akipiga gitaa la solo, Nkulu Wabangoi, Mbuya Makonga Adios, Ilunga Ngoe Bizos na wengine kadha.

Mchanganyiko huu hatari uliingia Studio muyda mfuoi baada ya kufanya mazoezi makali, iliikuwa ni Tarehe 26.1.1978 iliporekodi vibao vitano walivyovipiga katika mtindo wao mpya wa Kamanyola Bila jasho. Nyimbo hizo ni Nasema Sina ndugu, HOngera CCM, Kasongo Rudi Kijijini, Krismas na Uniachie ni wangu, moto wa nyimbo hizi baada ya kupigwa katika vipindi vya Redio Tanzania kishindo chake wala hakielezeki.

Umati wa watu walipewa heshima ya ya kuitwa Mzazi, Mlezi wa Marquiz walikuwa wakifurika katika ukumbi wa White House eneo la Ubungo Dar es Salaam na kumbi nyingine mbalimbali zilizokuwa zikipata bahati ya kutumbuiwa na bendi hiyo.

Ukumbi mwingine uliokuwa ukipokea idadi kubwa ya mashabiki ulikuwa ni Wapiwapis uliokuwa maeneo ya Chang'ombe na nyingine kadha.

Kuanzia muda huu na hata bendi hiyo kupitia misukosuko ya kuondokewa na wanamuziki mbalimbali kama vile Kiki na wengine.

Ushahidi wa kuendelea kuimarika kwa bendi hiyo ni ile albam waliyoirekodi muda mfupi baada ya King Kiki kuondoka na kujiunga na Orchestra Safari Sound, miamba hiyo ikaingia Studio Tarehe 24.11.1980 na kuachia nyimbo kali na za hatari kama Kiongo, Maiga, Pondamali, Pongezi Jeshi, Kidumu Chama Cha Mapinduzi, Zowa na Pongezi kwa viongozi.

Kundi hili kama zilivyo bendi nyingine limewahi kukumbana na misukosuko ya kibiashara na uendeshaji pia athari za vifo vuya wanamuziki wengi, lakini liliendelea kudumu hadi kwenye miaka ya mwisho ya 1990.

Ukiangalia albam za mwisho mwisho mfano ile iliyorekodiwa Tarehe 16.11.1989 ikiwa na nyimbo kama Ossa, Mashoga, Kisebengo, Tipwatipwa, Hali Ngumu, Marusu, Ndoa ya mateso, Mangolibo, HOngera Salim Ahmed salim, utaona bado ilikuwa imara licha ya kuwa na wanamuziki wengi chipukizi.

Kipindi hicho bendi hii ilisajili wanamuziki wengi chipukizi enzi hizo kama vile Burhan Adinani (Muba), aliyekuwa akipiga gitaa la solo, Kaingilila Maufi (Solo Namba mbili), MBwana Kocks aliyekuwa akipiga solo, Dekula Vumbi Kahanga (Solo) waliweza kuendeleza jahazi la bendi hiyo hadi lilipoingia kundi jingine la wanamuziki watatu Mpiga Solo Mutanachachou Kivukutu, Bobo Sukari na Fredito Butamu na kuasisi mtindo mpya wa Washawasha, kwa ufuoi bendi hiyo haikuwahi kufeli kuhusu nyimbo wala chaguo la wanamuziki.

Habari njema ni kwamba bendi hiyo sasa imerudi huku kiongozi wake Mkuu Nguza Vicking akikaribisha wadau kuibeba ili iweze kurudia makali yake kama ilivyokuwa enzi za nyuma, Tayari bendi hiyo inafanya maonyesho yake kila siku za Ijumaa katika ukumbi wa Polisi Mess Oster Bay.

Ina baadhi ya wanamuziki kama Nguza, Mukumbule Parashi, Kanku Kelly, Kasongo pascal Kalembwe, ASkulyake Saleh King Maluu na wengine kadha.



JAMVI LA HABARI
SPOTI
JUMATATU FEBRUARI 10, 2025



Mzee Nguza alirudisha Marquiz Og

>> Soma Uk. 15

# YANGA KUFA NA KUPONA NA JKT



NA MWANDISHI WETU

YANGA leo itakuwa na kibarua kizito itakapoivaa JKT Tanzania katika Uwanja wa Jenerali Isamuhyo, Mbweni Jijini Dar es Salaam, huku mahasimu wao Simba wakitamani kuona wapinzani wao hao wakipoteza mechi hiyo.

Simba wanaitazama kwa jicho la tamaa mechi hiyo huku wakielekeza dua zao kwa kikosi cha JKT kiweze kuibuka na ushindi ili kuwasimamisha mabingwa hao watetezi, wawe na uwiano mdogo wa tofauti ya pointi.

Yanga hadi sasa inaongoza Ligi ikiwa na pointi 45 ambazo ni pungufu ya pointi moja dhidi ya watani wao Simba yenye Pointi 44 baada ya kutoa sare 1-1 mechi yao iliyopita dhidi ya Fountain Gate, mchezo uliopigwa mjini Manyala.

Endapo Yanga itaibuka na ushindi leo itaizidi Simba Pointi 4 na hivyo kuwaacha mbali katika mbio za ubingwa wa Ligi ya NBC msimu huu, ambazo Wekundu hao wa Msimbazi wameapa kuzipigania kufa na kupona.

Yanga wataingia uwanjani hapo wakiwa na tahadhali kubwa, huku kocha wake mpya Miloud Hamd aliyerithi mikoba ya Sead Ramovic akiisimamia timu hiyo kwa mara ya kwanza.

## Ladack Chasambi aigawa Simba

NA MWANDISHI WETU

KINDA la Msimbazi aneyekuja vizuri katika medani ya Soka la Tanzania Ladack Chasambi, bado yupo katika wakati mgumu akipokea hisia tofauti kutoka kwa mashabiki baada ya kuisababishia timu yake kutoa sare 1-1 dhidi ya Fontain Gate mmchezo uliopigwa Jumatano iliyopita.



Chasambi alifunga bao katika harakati za kumrudhishia kipa dakika za mwicho za mechezo huo wakati timu yake ikiwa mbele kwa bao 1-0.

Kufuatua tukio hilo lililomfedhehesha chipukizi huyo kiasi cha kutoa machozi uwanjani, mashabiki wa timu hiyo wamegawanyika baadhi wakiwa upande wa Chasambi kuwa alifanya tukio hilo kwa makosa, wengine wakimkalia kooni wakidai kuwa lilikuwa ni tukio la kusudi.

Wanaomlaumu Chasambi ni baadhi ya mashabiki wenye msimamo mkali ambao wanadai kwamba dogo huyo, amevuruga mikakati yao ya kuwaporomosha mahasimu wao Yanga ambapo kama wangeshinda mecho ule wangewazidi kwa pointi moja.



## Kibu Denis bado aipasua Simba SC

**BAADA YA** kuikabili wenyeji wao Foutain Gate katika uwanja wa Tanzanite Kwaraa ulioko Babati mkoani Manyara, Wekundu wa Msimbazi wamekataa kumuuza nyota wao, Denis Kibu, kwa MC..

>> Inaendelea Uk. 14

GAZETI HILI HUTOLEWA NA JAMVI MEDIA GROUP, S. L. P 78862, DAR ES SALAAM